# Mama Mwinyi ahimiza kusaidia wazee na watoto ..Uk.3

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

**Tanzania BORA**

Ni Mimi na Wewe

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz | ISSN 4256-1873 Toleo Na.38 Tanzania Bora ALHAMISI Machi 06, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100


UK.15

Tanzania BORA MICHEZO

ALHAMISI Machi 06, 2025 Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz

Simba yamtolea macho mwamuzi

NA MWANDISHI WETU

HAKUNA ubishi kwamba Simba na Yanga ni rasmi sasa zitaonyeshana ubabe katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC, utakaopigwa Jumamosi Machi 8, huku mwamuzi wa mchezo huo akitajwa kuwa ni Ahmed Arajiga.

Inaendelea Uk.14

TIKETI MECHI YA SIMBA, YANGA ZAADIMIKA MTAANI

NA MWANDISHI WETU

Inaendelea Uk.14

KASEJA APEWA KIBARUA KIZITO KAGERA SUGAR

NA MWANDISHI WETU

Inaendelea Uk.14

# Dk. Mpango atoa ushauri muhimu

HABARI UK.2

>> Afungua Mkutano wa 11 wa Petroli wa Afrika Mashariki Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere

>> Ataka Mataifa ya Afrika Mashariki yashirikiane ili kunufaike na sekta ya nishati ambayo inaendelea kukua kwa kasi

>> Dkt. Biteko amshukuru Rais Dkt. Samia kwa jitihada za kuendeleza mkondo wa juu kwa lengo la kugundua vyanzo vya gesi hapa nchini

*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Gesi Asilia wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) Dkt. Esebi Nyari kuhusu namna ya matumizi ya gesi katika vyombo vya moto wakati wa kukagua mabanda ya maonesho katika Mkutano wa 11 wa Petroli wa Afrika Mashariki unaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC). jana Tarehe 05 Machi 2025.*






# Trump aonya maandamano, asema ndiyo kwanza anaanza

NA MWANDISHI WETU

KATIBU wa Uenezi na Mafunzo wa CCM CPA Amos Gabriel Makala alisema kuwa viongozi wa Chamdema kuanzia Mwenyekiti wao Tundu Lisu na wenzake wote, hakuna hata mmoja mwenye ubavu wa kuzuia kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu nchini hapo mwezi Oktoba mwaka huu.

Akizungumza katika mkutano wa viongozi wa chama na jumuiya ngazi ya shina, tawi, kata na wilaya katika Wilaya ya Kinondoni mkoani Dar es salaam

Inaendelea Uk. 3

# Dk. Samia aleta matumaini makubwa upatikanaji maji

HABARI UK.2



# DK.MPANGO ATOA USHAURI MUHIMU

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango ametoa wito wa kuimarishwa ushirikiano zaidi kwa Mataifa ya Afrika Mashariki ili kuweza kunufaika na sekta ya nishati ambayo inaendelea kukua kwa kasi.

Makamu wa Rais ametoa wito huo wakati akifungua Mkutano wa 11 wa Petroli wa Afrika Mashariki unaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

Amesema ni muhimu kuungana pamoja kuweza kutumia rasilimali iliyopo katika sekta ya nishati Afrika Mashariki na kutengeneza njia ya maendeleo endelevu na ustawi wa kudumu wa ukanda huo. Pia amewakaribisha wawekezaji na wadau wa maendeleo kuungana na Mataifa ya Afrika Mashariki katika kuendeleza sekta hiyo.

Makamu wa Rais amehimiza majadiliano katika Mkutano huo yaweze kusaidia katika sera za mataifa husika kwa maendeleo endelevu ya sekta ya nishati. Amesema ni lazima kuendelea kuhamasisha uhamaji wa haki kuelekea katika matumizi ya nishati safi na kuhakikisha athari za kiuchumi na kijamii za mabadiliko hayo zinakuwa sawa kwa watu wote na kila mmoja ananufaika na mabadiliko kuelekea matumizi ya nishati safi bila kuachwa nyuma.

Makamu wa Rais amesema ni muhimu kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kutumia kwa ufanisi rasilimali zote za nishati ikiwemo mafuta ili kuweza kukabiliana na upungufu wa nishati kutokana na kuongeza kwa mahitaji hayo katika kufikia maendeleo kwa haraka. Ameongeza kwamba rasilimali za nishati zitaweza kuwa chanzo kikuu cha mapato kwa serikali na hivyo kusaidia katika uwekezaji kwenye miundombinu na huduma za kijamii na kuunga mkono ajenda nzima ya maendeleo.

Amesema Afrika Mashariki imejaaliwa rasilimali kubwa ya nishati ikiwemo mafuta huku mataifa yakiwa na ugunduzi mbalimbali kama vile kugunduliwa kwa gesi asilia nchini Tanzania, mafuta nchini Uganda, Kenya na Sudan, Methane kwa nchi ya Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo pamoja na nishati ya jotoardhi kwa nchi za Tanzania na Kenya.

Halikadhalika Makamu wa Rais amesema maendeleo ya teknolojia ni fursa kwa nchi zinazoendelea kuongeza uwezo wa uvunaji endelevu wa nishati ya mafuta. Ameongeza kwamba ili na maendeleo endelevu ya sekta ya nishati ni muhimu mapato yanayotokana na uwekezaji huo yaweze kufadhili miradi mbalimbali ya maendeleo, kutengeneza ajira na uwekezaji katika jitihada za kurejesha mazingira yaliyoharibiwa.

Amesema ni vema sera na sheria kujumuisha utengaji wa asilimia kadhaa ya mapato yatokanayo na rasilimali ya mafuta kwaajili ya matumizi ya baadae.

Kwa upande wake Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Doto Biteko amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada za kuendeleza mkondo wa juu kwa lengo la kugundua na kuendeleza vyanzo vya gesi hapa nchini. Amesema katika uongozi wake kwa upande wa mkondo wa juu hatua muhimu imefikiwa ikiwemo kuimarisha uzalisha wa gesi asilia katika vitalu ya Songosongo na Mnazi bay ambavyo kimsingi ni maendeleo kwenye uchumi wa gesi.

Aidha Dkt. Biteko ameongeza kwamba maendeleo mengine ni pamoja na kuongezeka kwa ushiriki wa kampuni ya Serikali ya TPDC katika kitalu cha Mnazi bay kutoka ushiriki wa asilimia 20 hadi asilimia 40.




# MAMA MWINYI AHIMIZA KUSAIDIA WAZEE NA WATOTO

NA MWANDISHI WETU

MKE wa Rais wa Zanzibar, Msarifu na Mwenyekiti wa Bodi ya wadhamini ya Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF), Mhe.Mama Mariam Mwinyi ametoa rai kwa wadau mbalimbali kuwasaidia Watoto na Wazee wenye mahitaji Maalum katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mariam Mwinyi aliyasema hayo alipovitembelea Vituo vya kuwalea Watoto SOS, Mazizini na cha Wazee Welezo kuwapa msaada wa vyakula, Mkoa wa Mjini Magharibi jana.

Aidha, Mariam Mwinyi ameeleza kuwa ataendelea kuwasaidia zaidi Watoto na Wazee wenye mahitaji Maalum ikiwemo vyakula katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na Sikukuu ya Eid.

Mariam Mwinyi amewahimiza Watoto kuwa wenye tabia njema na kufanya ibada katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani .

Halikadhalika Mama Mariam Mwinyi amewasilisha salamu za upendo kutoka kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt.Hussein Ali Mwinyi katika vituo hivyo.

Naye, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto Zanzibar Mhe. Dkt.Riziki Pembe Juma amemshukuru Mama Mariam Mwinyi kwa kuendelea kuwajali Watoto wenye mahitaji Maalum katika vituo mbalimbali Zanzibar.

# MAJALIWA ALETA MATUMAINI MAKUBWA UPATIKANAJI MAJI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, jana Machi 05, 2025 ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi wa Bwawa la Kidunda litakalokuwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita bilioni 190 ambalo linatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 335.8 hadi kukamilika kwake.

Akizungumza na wakazi wa kijiji cha Kidunda, Wilayani Morogoro, Mheshimiwa Majaliwa amesema kuwa ujenzi wa bwawa hilo ambao umefikia asilimia 28. Ujenzi huo ni utekelezaji wa maono ya Hayati baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere ambaye alidhamiria kulijenga ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro.

"Bwawa hili lilikuwa katika historia tangu Serikali ya awamu ya kwanza na zilizofuatia, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya kuhakikisha maji ya kutosha yanapatikana, alielekeza kuanza kutekelezwa kwa mradi huu, na leo tumeweka jiwe la msingi, na anamatarajio makubwa na mradi huu."

Mheshimiwa Majaliwa ameongeza kuwa ujenzi wa bwawa hilo ni utekelezaji wa dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha anamtua mama ndoo kichwani kwa kufikisha huduma ya maji safi na salama karibu na makazi ya wananchi.

Kadhalika Mheshimiwa Waziri Mkuu ameziagiza Mamlaka za Maji ziendelee kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa na Serikali kwa gharama kubwa iweze kuwa endelevu.

Pia, Mheshimiwa Majaliwa alisisitiza kuwa Wizara ya Maji ihakikishe inamsimamia mkandarasi ili mradi huo ukamilike kwa wakati "Tunataka mradi huu ukamilike kwa wakati, hatuna shaka na mkandarasi huyu, amefanya miradi mingi na kwa ufanisi".

# WAFANYAKAZI TRA WAPEWA ANGALIZO

NA MWANDISHI WETU

KAMISHINA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Bw. Yusuph Juma Mwenda amewataka watumishi wa Mamlaka hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii ili kuendeleza rekodi nzuri ya makusanyo iliyowekwa kwa kipindi cha miezi nane mfululizo ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Kamishna Mkuu Mwenda amewapongeza Watumishi wa TRA kwa kuendelea kufanya kazi kwa bidii na kuimarisha uhusiano na Walipakodi ambao Imani yao kwa TRA imezidi kuongezeka na kuchochea ulipaji wa kodi kwa hiari.

Kamishna Mkuu Mwenda amesema wapo baadhi ya Watumishi ambao wamekuwa wakilalamikiwa na Walipakodi kwa tuhuma mbalimbali ambazo zimekuwa zikichunguzwa kikamilifu na kuwahakikishia kuwa hakuna Mtumishi atayechukuliwa hatua kwa uonevu.

Amewataka kuzingatia maadili katika utekelezaji wa majukumu yao ili kuondoa malalamiko kutoka kwa baadhi ya Walipakodi.

Kamishna Mkuu Mwenda amewataka Watumishi hao kuendelea kuzingatia na kutekeleza maelekezo mbalimbali yanayotolewa na viongozi likiwemo agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan la kutaka kusimamia ulipaji wa Kodi kwa hiari.

Kamishna Mkuu Mwenda amesema mbali na hayo Rais Samia amekuwa mstari wa mbele kutoa maelekezo ya kuhakikisha kila anayestahili kulipa kodi analipa na kuwachukulia hatua wale wanaojihusisha na ukwepaji wa Kodi kwa namna mbalimbali jambo ambalo linapaswa kusimamiwa na kila mmoja ndani ya TRA.

Amesema kufuatia maelekezo hayo na miongozo inayotolewa wameweza kuongeza makusanyo ya kodi na kuvuka malengo waliyowekewa na Serikali kwa miezi Saba mfululizo na kuwataka watumishi wa TRA kuendelea kuzingatia maelekezo hayo ili waendelee kuvunja rekodi ya makusanyo.

Kamisha Mkuu Mwenda ametaja miongoni mwa mambo yaliyowezesha kuvuka malengo kwa miezi Saba mfululizo kuwa ni pamoja na ulipaji wa Kodi wa Hiari unaohusisha utolewaji wa Elimu kwa Mlipakodi na ziara za Viongozi kuwafuata Walipakodi na kuwasikiliza hali ambayo imewezesha kutatuliwa papo kwa hapo kwa changamoto za Walipakodi.

"Pamoja na wenzangu ndani ya TRA wakiwemo mameneja wa mikoa tumekuwa na utaratibu wa kuwafuata Walipakodi na kuzungumza nao katika maeneo yao hii imetusaidia sana kutengeneza uhusiano wa karibu na Walipakodi, na Mimi binafsi nimepita mikoa yote na nimekutana na Walipakodi" amesema Kamishna Mkuu Mwenda.

Amesema uhuru uliotolewa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa TRA kufanya kazi zao bila kuingiliwa unapaswa kutumiwa ipasavyo kwa watumishi kujituma na kuhakikisha mianya yote ya ukwepaji kodi inazibwa hali ambayo itaendelea kuimarisha makusanyo ya kodi na kuleta usawa katika kukusanya Kodi.

Kamishna Mkuu Mwenda amesema mapambano dhidi ya wakwepa Kodi yanapaswa kuongezeka ili kutowaumiza walipakodi waaminifu ambao wamekuwa wakifanya kazi zao katika sehemu moja na wasiolipa kodi jambo ambalo linapunguza ushindani wa kibiashara hali inayoweza kuua Biashara za Walipakodi waaminifu.

Awali akizungumza katika kikao hicho, Naibu Kamishna Mkuu wa TRA Bw. Mcha Hassan Mcha amesema Baraza la Wafanyakazi ni chachu ya kuboresha utendaji kazi na kuwa kwa kipindi cha muda mfupi ambao Baraza hilo limekuwepo, manufaa yake yameonekana.

TRA
NZANIA REVENUE AUTHORI
ISO 9001: 2008 Certified

## WAZIRI MKUU AZUNGUMZIA NNYENZO YA KUPUNGUZA UMASIKINI

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, amesema kuwa huduma jumuishi za kifedha ni kiungo muhimu cha ukuaji wa uchumi, kupunguza umasikini na kuchochea maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Alisema Serikali kwa kutambua hilo imedhamiria kuendelea kushirikiana na wadau wote ili kuhakikisha sekta ya kifedha inazidi kuwa jumuishi, fanisi, na yenye tija kwa maendeleo ya Taifa.

Alisema hayo alipozindua huduma mpya za kidijitali za Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) katika ukumbi wa Super Dome, Masaki jijini Dar es Salaam.

Ameongeza kuwa katika vipindi tofauti, Serikali imekuwa ikiandaa na kutekeleza mikakati ya Taifa ya kuboresha huduma jumuishi za kifedha.

"Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa 2023 - 2028 ni mwendelezo wa mafanikio yaliyopatikana kupitia Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha uliokamilika Desemba 2022"

Kadhalika, Mheshimiwa Majaliwa alisema kuwa jitihada nyingine ni kuandaa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa miaka 10 kuanzia mwaka 2024 hadi 2034. "Mkakati huu umeainisha malengo mahsusi ambayo kama nchi tunaazimia kuyatekeleza ili kufikia uchumi wa kidijitali."

Kwa upande wake, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Sauda Msemo alisema sekta ya fedha imeendelea kuwa na ustahimilivu na hivyo kuwezesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kufanyika.

Aidha, Naibu Gavana huyo ametoa wito kwa taasisi zote za kifedha zifuate viwango bora vya usalama wa mitandao na kugundua haraka pale panapotokea udanganyifu wa aina yoyote.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi alisema lengo la uzinduzi wa huduma hizo za NBC kidijitali ni kuboresha utoaji wa huduma za kifedha na kuzifanya zipatikane kwa urahisi. "Huduma hizo ni pamoja na ufunguaji wa akaunti, kuhamisha fedha, kupata mikopo bila ya kwenda katika tawi."

Mradi huo utakapokamilika unatarajia Kuboresha huduma ya Majisafi kwa ajili ya matumizi ya Majumbani, Kilimo na Viwanda kwa kuhakikisha upatikanaji wa muda wote katika mto Ruvu kwa kutiririsha wastani wa lita 24,000 kwa sekunde zitakazokidhi mahitaji ya maji hususani kwenye kipindi cha ukame.

# JAMII YAKUMBUSHWA UMUHIMU WA KUENZI HISTORIA



NA MWANDISHI WETU

JAMII imetakiwa kuthamini utalii wa ndani, malikale pamoja na kuenzi mchango wa makumbusho ya majimaji katika kujenga na kuhifadhi historia ya nchi.

Hayo yamebainishwa na Katibu Tawala Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma Francis Mgoloka wakati akisoma hotuba kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Ngollo Malenya kwenye tamasha kuhusu mila na desturi lililoandaliwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Makumbusho ya vita ya majimaji ili kuwaenzi waliouawa wakati wa vita ya majimaji.

Mgoloka alisema ili kutimiza azma ya kutumia makumbusho kama chachu ya utalii, ni muhimu jamii ikathamini utalii wa ndani na kutunza malikale zilizopo.

"Wakati ni sasa wa kubadili mitazamo yetu kuona utalii si tu wa kufanywa na watu kutoka nje bali pia tunaweza kufanya utalii wa ndani ambao utakuza utamaduni wetu kwa kujifunza na hivyo kusaidia kukuza urithi wa utamaduni wetu," alisema Mgoloka na kuongeza

"Kama kauli mbiu inavyosema ni wakati muafaka wa kutumia makumbusho haya kama chachu ya maendeleo kupitia utalii wa utamaduni, makumbusho ni sehemu muhimu za historia ya Tanzania kwa vizazi vya sasa na vijavyo kujifunza," alisisitiza.

Alisema makumbusho ya Majimaji ni miongoni mwa makumbusho saba ya taifa yaliyopo nchini Tanzania yakitumika kuhifadhi historia ya nchi na kutoa elimu kwa jamii ili itambue inakotoka wapi, ilipo na inapokwenda.

Kwa upande wake, Kaimu Mhifadhi Mkuu wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Makumbusho ya Taifa, Frola Vicent amesifu mwitikio wa wananchi katika tamasha hilo llitakalofikia kilele chake Februari 27, 2025 akisema mwamko unaongezeka kila mwaka.

Alisema moja kati ya sababu za kukubalika kwa tamasha hilo ni ushirikishwaji wa moja kwa moja wa wazee wa kimila na machifu wa makabila ya kusini mwa Tanzania ambao ndio waliopigana vita enzi hizo wakitumia silaha za jadi.

Kama sehemu ya ushirikishwaji huo, Vicent alisema walifanya uamuzi wa makusudi wa kupeleka shughuli za tamasha hilo katika wilaya za mkoa huo ni kuwajengea uwelewa wananchi na kuwahamasisha kutembelea Makumbusho ya Majimaji ili kujifunza na kufahamu historia ya nchi.

"Awali midahalo hii ilikua inafanyika katika eneo moja tu, tofauti na sasa ambapo umekuwa ukifanyika katika kila Wilaya za Mkoa wa Ruvuma, ambapo mwaka 2024 ulifanyika Wilayani Nyasa, na leo tupo hapa Wilayani Namtumbo.," alisema Frola

Naye Mhifadhi Mambo ya Kale Mwandamizi wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Rahel Kisusi alisema tamasha hilo ni fursa sio tu kwa watanzania bali dunia nzima kutafakari mchango mkubwa uliotolewa na mashujaa wazalendo katika kupigania utu na heshima ya watanzania na waafrika.

Kisusi pia alifafanua kuwa tamasha hilo ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuhakikisha malikale na historia nchini zinatumika kwa maendeleo ya utalii na uchumi wa Taifa.

"Wizara inaendelea kuchukua hatua madhubuti zikiwemo kuimarisha uhifadhi na uendelezaji wa makumbusho na maeneo ya kihistoria; kushirikiana na sekta binafsi na wadau mbalimbali wa maendeleo; kuhamasisha tafiti na elimu kuhusu vita vya Majimaji na historia nyingine muhimu; na kuongeza juhudi za utangazaji wa maeneo ya kihistoria kama vivutio vya utalii." Alisisitiza Kisusi.

Tamasha hilo lenye kauli mbiu ya "Makumbusho ya Majimaji na Malikale zetu, kwa Maendeleo ya Utalii na Uchumi" lina dhima ya kuenzi mashujaa walipigania uhuru wa Tanzania dhidi ya wakoloni wa Ujerumani katika vita ya Majimaji iliyopigwa kuanzia mwaka 1935 – 1937 vikijumuisha jamii 21 katika mikoa saba ya Kusini mwa Tanzania, Ruvuma ikiwa mojawapo.




# WAZIRI JAFO ATAKA MISINGI SAHIHI KUTIMIA MALENGO

NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Mhe. Dkt, Suleimani Jafo (Mb) ameiagiza Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO) kuhakikisha inatengeneza misingi sahihi ya upatikanaji fedha ili kutimiza malengo ya Taasisi hiyo katika kukuza wa uchumi wa viwanda.

Dkt. Jafo ameyasema hayo wakati wa uzinduzi Bodi ya Wakurugenzi wa TEMDO uliofanyika katika Taasisi hiyo jijini, Arusha.

Aidha amesema Wizara yake itashirikiana na Wizara ya Afya na TAMISEMI ili kuhakikisha taasisi za umma zinanunua vifaa tiba vinvyotengenezwa na TEMDO ili kuokoa fedha nyingi inayotumika kuagiza vifaa hivyo nje ya nchi.

Vilevile ameishauri Bosi hiyo kushirikiana na taasisi nyingine kama vile Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) na nyinginezo ili kupata fedha za kuendeleza miradi mbalimbali itakayoanzishwa katika Taasisi hizo.

Katika Hatua nyingine amewasihi Wajumbe hao wa Bodi pamoja na Watumishi wa TEMDO kufanya kazi kwa bidii, weledi, uadilifu, ubunifu na upendo ili kuleta tija na ufanisi katika utendaji kazi na utoaji huduma kwa ummakutimiza malengo ya Taasisi hiyo katika kuleta taswira nzuri ya kuhakikisha maendeleo ya TEMDO yanakuwa.

Naye, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dkt Hashil Abdallah ameisisitiza Bodi hiyo kuhakikisha maendeleo ya viwanda yanakua ikiwemo utekelezaji wa Sera sanjari na kubuni miradi mbalimbali.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Temdo, Kanali Mstaafu Joseph Simbakalia ameahidi kuwa Bodi hiyo itafanya kazi kwa bidii katika kukuza maendeleo ikiwemo kubuni miradi yenye kuleta mapinduzi katika sekta ya viwanda.

Awali Mkurugenzi wa TEMDO, Prof Frederick Kahimba amesema , TEMDO imetengeneza na kusambaza vifaa tiba 2,262 vya aina mbali mbali ikiwemo vitanda, kabati za wodini, standi ya drip, vitanda vya mama wajawazito, vitanda vya uchunguzi, jokofu za kuhifadhia maiti na vichomea taka hatarishi.

Kwa upande mwingine katika kuhakikisha Wizara ya Viwanda na Biashara inafikia malengo yake safari hii imekuja na mikakati minne yenye lengo la kuimarisha mfumo wa stakabadhi ghalani kwa msimu wa mwaka 2025/26.

Hayo yalibainishwa wa Waziri Jafo, katika kuimarisha mfumo huo, wizara kupitia Bodi ya Stakabadhi za Ghala (WRRB), ambapo ilipanga kuendelea kuboresha mfumo huo kwa kupanua utekelezaji wake katika maeneo mapya ili kuongeza tija kwa wakulima na wadau wa sekta ya kilimo.

Waziri Dk Jafo alisema kuwa kupitia bodi, juhudi za kuhamasisha matumizi ya mfumo huo zitaimarishwa sambamba na kutatua changamoto na kero zilizojitokeza msimu uliopita.

Pamoja na hayo pia kuna mikakati mingine kwa mujibu wake ni bodi kukamilisha kwa haraka mchakato wa kupata ithibati ya Benki Kuu

juu ya mwongozo utakaosimamia utendaji wao ili uanze kutumika kwa lengo la kuondoa changamoto ya hasara ambazo baadhi ya taasisi za fedha zimekuwa zikikutana nazo.

Alisema pia kupanua matumizi ya Meneja Dhamana hususani katika biashara ya nafaka ili kuchochea usindikaji wa mazao, kuongeza thamani na kuimarisha ajira katika maeneo ya vijijini, na kuendeleza urasimishaji wa bidhaa mpya na ambazo hazijatumia kikamilifu mfumo ikiwamo zao la kahawa.

Alisisitiza na kuwakaribisha wadau hususani sekta binafsi, halmashauri za miji, manispaa na majiji kuwekeza katika ujenzi wa ghala za kisasa katika maeneo yanayotekeleza mfumo wa stakabadhi za ghala.

Mikakati hii iliyotajwa na wizara ni muhimu na imekuja katika wakati mwafaka kutokana na ukweli kwamba stakabadhi ya mazao ghalani imefanya vizuri katika maeneo na mazao ambayo yalianza kutumia mfumo huu.

Miungoni mwa mafanikio ya mfumo ni mauzo ya mazao hayo kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala yamesaidia upatikanaji wa bei nzuri ya soko kutokana na ushindani wa wanunuzi na hivyo kuwanufaisha wakulima wa maeneo husika.

Mfano ni bei ya kakao kabla ya mfumo ilikuwa Sh 2,500 na baada ya mfumo bei ilikuwa Sh 32,000 kwa kilogramu; ufuta bei kabla ya mfumo ilikuwa Sh 500 hadi Sh 800 baada ya mfumo bei iliongezeka na kuwa Sh 2,800 hadi Sh 4,500 kwa kilogramu.

Kama ilivyo kazi ya WRRB ya kusimamia na kuhamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani unaohakikisha usawa na uendelevu wa upatikanaji wa mikopo na mifumo ya masoko, tunafarijika kuona serikali inazidi kuweka mikakati ya kuimarisha mfumo na kutanua wigo kwa kurasimisha bidhaa mpya.

Ni imani yetu kwamba Bodi ya Stakabadhi ya Ghala itasimamia kikamilifu utekelezaji wa mikakati hii ili kuja na matokeo chanya na kusaidia wakulima na taifa kwa ujumla katika masuala ya masoko na uuzaji wa mazao, na hivyo kuchangia kukuza uchumi.

# TUME HURU YA UCHAGUZI YATAJA IDADI YA WAPIGA KURA DAR

NA MWANDISHI WETU

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) imetangaza mpango wa kuandikisha wapiga kura wapya 643,420 jijini Dar es Salaam kati ya Machi 17 na 23, 2025.

Hata hivyo, wadau wa uchaguzi wameanza kuhoji ufanisi wa zoezi hilo, wakitaka uhakika wa usimamizi mzuri na uwazi wa mchakato huo.

Akizungumza jana Mwenyekiti wa Tume, Jaji wa Rufani Jacobs Mwambegele, amesema uandikishaji huo ni sehemu ya awamu ya kwanza ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ambalo limekwisha kufanyika katika mikoa 28 nchini.

“Tume inatarajia baada ya uandikishaji, Mkoa wa Dar es Salaam utakuwa na wapiga kura 4,071,337, lakini idadi hii inaweza kuongezeka endapo wapo waliostahili kujiandikisha lakini hawakufanya hivyo mwaka 2019/20,” alisema Mkurugenzi wa Uchaguzi, Kailima Ramadhan.

Licha ya mipango hiyo, baadhi ya wadau wameeleza mashaka juu ya muda mfupi wa zoezi hilo, wakisema siku saba pekee huenda zisitoshe kuhakikisha kila mwenye sifa anapata nafasi ya kujiandikisha. Aidha, swali limeibuka kuhusu ufanisi wa vituo 1,757 vilivyotengwa, ikizingatiwa kuwa ni ongezeko dogo la vituo 96 tu ikilinganishwa na mwaka 2019/20.

“Tuna wasiwasi na maandalizi haya, hasa kwa idadi kubwa ya watu Dar es Salaam. Je, vifaa vya kutosha vipo? Je, watumishi wa Tume wako tayari kuhakikisha kila mwenye haki anajiandikisha bila changamoto?” amehoji mdau mmoja wa uchaguzi ambaye hakutaka kutajwa jina lake.

Pamoja na hilo, Tume imetangaza kuwa itatoa nafasi kwa waliopoteza kadi zao, waliohama maeneo yao, na wale wanaotaka kurekebisha taarifa zao. Hata hivyo, bado haijaweka wazi mikakati madhubuti ya kuhakikisha kila hatua inatekelezwa kwa uwazi na bila upendeleo.

Je, Tume itaweza kusimamia zoezi hili kwa ufanisi na kuhakikisha kila mwenye haki anajiandikisha bila vikwazo? Wadau wa uchaguzi na wananchi wanaendelea kufuatilia kwa karibu maendeleo yake.

Akiwasilisha mada kwenye mkutano huo, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Ndugu. Kailima Ramadhan amefafanua kuwa kwa mkoa wa Dar es Salaam Tume inatarajia kuandikisha wapiga kura wapya 643,420 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 18.7 ya wapiga kura 3,427,917 waliopo kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

# MASOKO YA MADINI YAZIDI KUINEEMESHA NCHI



NA MWANDISHI WETU

WAKATI masoko ya madini yakifikia 43, mchango wa masoko hayo umeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 8 mwaka 2018/ 2019 hadi Shilingi Bilioni 183 mwaka wa fedha uliomalizika wa 2023/2024.

Akizungumza katika mafunzo ya matumizi ya mashine maalum ya kupima madini ya metali kwa njia ya MIONZI /X-RAY, kwa maafisa masoko wa madini Mkurugenzi wa Ukaguzi na Biashara ya Madini, Venance Kasiki amesema mbali na masoko hayo pia kuna vituo vya ununuzi wa madini 109.

Amesema, "Kwa kuzingatia asilimia kubwa ya mapato yetu katika masoko yanatokana na madini ya dhahabu, na ili tupate maduhuli lazima tutumie mashine za XRF kupima asilimia (purity) ya madini yanayouzwa. Majibu yanayotokana na XRF yanatumika kukokotoa mrabaha na ada ya ukaguzi,".

> Amesema, ni imani yake kuwa baada ya mafunzo hayo vifaa vitatumika kwa usahihi, tija na kasi ya ukusanyaji maduhuli itaongezeka.

Kwa upande wa Meneja wa Biashara ya Madini Sundi Malomo akizungumza amesema kuwa tangu Serikali kupitia Tume ya Madini kuanzisha masoko ya madini Mei, 2019 kama mkakati wa kuimarisha biashara ya madini nchini, masoko hayo yamekuwa na mchango mkubwa wa kuongeza mapato ikiwemo kutoa ajira.

"Ili kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kama mnavyofahamu Sekta ya Madini inatakiwa ichangie asilimia 10 katika Pato la Taifa kwa mwaka wa Fedha 2024/2025, Tume ya Madini imepewa lengo la kukusanya Shilingi Trilioni 1, hivyo tumewapa mafunzo maafisa masoko na kuwakumbusha majukumu ya Idara- sehemu ya biashara," amesema Sundi na kuongeza.

" Katika mafunzo haya tumeweza kuainisha changamoto tulizonazo na kuweza kuonyesha mchango wa masoko kuanzia mwaka 2018/2019 ambapo mchango wa masoko ulikuwa ni Shilingi Bilioni 8, mchango huo umeongezeka kwa kiasi kikubwa mwaka hadi mwaka, mwaka wa fedha 2023/2024 masoko haya yameweza kuchangia takribani Shilingi Bilioni 183," amesema Sundi.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi wa Ukaguzi na Biashara ya Madini, Venance Kasiki amesema ili kuhakikisha mashine za XRF zinatumika vizuri na lengo kusudiwa linapatikana, wameamua kufanya mafunzo kwa watumiaji wa vifaa hivyo waliopo kwenye masoko ya madini mikoa yote ya Tanzania Bara .

Aidha, amesema wamemualika mtaalam kutoka Kampuni ya Thermo Fisher Scientific ya Afrika Kusini ambao ndio watengenezaji wa mashine hizo, Mirko Steinhage kutoa elimu zaidi juu ya matumizi sahihi ya XRF.

Kwa upande wake Kaimu Meneja Ukaguzi Madini na Huduma za Maabara, Mhandisi Mvunilwa Mwarabu amesema mafunzo hayo ni fursa njema kwa kuwa mashine za XRF na Mizani ndio vinasaidia katika ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali hivyo ni muhimu zikatumika kwa ubora ili kubaini kiasi sahihi cha madini na Serikali ipate mapato yake sahihi.

Amesema, ni imani yake kuwa baada ya mafunzo hayo vifaa vitatumika kwa usahihi, tija na kasi ya ukusanyaji maduhuli itaongezeka.

# TAHARIRI

## Usimvunje nguvu mkuu wa nchi anapowaza kutukomboa

KUMEKUWA na maneno ya chini chini kwenye mitandao ya jamii juu ya ziara anazofanya Rais Samia Suluhu Hassan kwenye mataifa mbalimbali duniani.

Ziara ambazo zinasaidia kuifungua nchi kimataifa, kuwapa fursa wawekezaji wa ndani kuona upeo wa dunia lakini pia kuweka mazingira mazuri ya kukaribisha wawekezaji wa nje.

Hata hivyo, wapo wanaoumizwa na ziara hizo. Kwa madai hazina maana, zinatumia fedha za walipa kodi bure bila sababu. Wanakwenda watu wengi kuliko ilivyopaswa kuwa.

Ni kauli za wakosaji, ambazo zimejaa hila, ghiba na choyo kisicho na sababu yoyote. Rais Samia Suluhu Hassan amekifanya kile ambacho viongozi wengi waliopata kukalia kiti chake nchini hawakuweza, au walikifanya kwa udogo.

Kitendo cha kuongozana na wafanyabiashara, wanahabari, wasanii, wanamichezo, wanamazingira na watu wa kada mbalimbali katika ziara zake ni upeo wa juu wa kuwafikiria wananchi wake.

Wanapofika huko watu hao ambao baadhi wanajigharamia nauli na malazi, wanatambulishwa kwa diaspora. Wanatambulishwa kwa wafanyabiashara wakubwa au wasanii wakubwa wa nchi anazotembelea Rais Samia.

Hakuna kitu kizuri kama kupata kiongozi anayefikiria hatma ya wananchi wake, angeweza kwenda mwenyewe kimya kimya kisha akarudi kimya kimya na chochote kisitokee. Lakini ameamua kulifanya hili la kuongozana na watu bado wapo wanaomsakama.

Hatumtendei haki, kwa sababu analifanya hili si kwa kushurutishwa na hakuna namna yoyote iwayo kuwa ananufaika na kitendo hiki zaidi ya kuwa wanaokwenda naye ndio wanaonufaika.

Kama hiyo haitoshi, mbali ya ziara za kitaifa anazofanya anapata wasaa wa kufuatilia mikopo na misaada yenye masharti nafuu kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwemo hospitali, miundombinu ya barabara, majengo na taasisi za elimu.


**BODI YA UHARIRI**

Mhariri Mkuu:
Mhariri Habari za Biashra & Uchumi:

Mhariri wa Habari:
Idara ya Masoko:

**MAWASILIANO**

JAMVI MEDIA GROUP





*Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Jaji wa Rufani Jacobs Mwambegele akizungumza jana wakati akifungua mkutano wa Tume na Wadau wa uchaguzi mkoa wa Dar es Salaam kuhusu Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. (Picha na INEC).*

# UCHAMBUZI

## Nchimbi -- mshikamano wetu ndio nguzo yetu

ANAANDIKA MSHITITI DK. AHMAD SOVU

KAMA angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu wa timu ya Yanga basi Dk. Nchimbi ningemuita Aziz Ki au wa Azam angekuwa Fei toto na kama ni Simba basi ndio Clatous Chama na kama ni Mashujaa basi ndio Reliants Lusajo. Maana amepiga ndipo palipo.

Kupiga huku si kupiga kwa boli hapana, ni kutoa hoja au ukumbusho katika wakati mwafaka na pahala mwafaka.

Akiwa mkoani Singida katika ziara yake ya kwanza kwa mzunguko huu wa pili wa mfululizo wa ziara zake, katibu mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi kwa kinywa kipana kabisa na bila kificho amekemea tabia ya baadhi ya watu wachache kutaka kutugombanisha na kuhubiri chokochoko na kauli za kibaguzi zinazoashiria kuvuruga umoja na mshikamano wetu kama taifa la Tanzania.

Alisema Dk. Nchimbi: "Tusikubali kuacha umoja wetu nawaombeni sana, kama kuna jambo mkienda nyumbani leo na mtu akikuuliza katibu mkuu amesema nini umwambie amesema tusikubali kuacha umoja wetu, tusikubali kugawanywa, tusikubali kufarakanishwa."

Kauli hii ya Dk. Nchimbi imekuja wakati mwafaka kwani ni kweli zipo bishara za baadhi ya watu kuanza maneno yanayoelekea kuuteteresha umoja wetu.

Watanzania ni wamoja na umoja na mshikamano wetu kwa hakika hauna mbadala.

Umoja na mshikamano wetu ndio umetufikisha katika hatua kubwa ya maendeleo iliyopigwa.

Tumeshuhudia mathalan, katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Rais Dk. Samia kumepigwa hatua kubwa za maendeleo.

Uendelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo kama vile SGR, umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya mwendokasi na barabara nchi nzima, ongezeko kubwa la watalii, maboresho makubwa katika sekta ya afya na elimu, maboresho katika sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo,michezo, sanaa mawasiliano n.k ni mifano ya umuhimu wa kuwa na umoja, amani na mshikamano kama Taifa.

Hivyo, ni lazima kulinda umoja huu na mshikamano wetu na kuepuka kubaguana kwa misingi ya ukabila, dini, maeneo na matabaka kama alivyosisitiza Dk. Nchimbi kuwa;

"Tanzania lazima iendelee kuwa nchi moja yenye mshikamano, yenye upendo ambayo haibagui watu wake kwa misingi ya ukabila, wala dini wala vyama vya siasa. Wote ni Watanzania, nchi yetu sote tuishi kwa kushirikiana na tupendane."

Kwa hakika, tunatoa kongole sana kwa Balozi Dk. Nchimbi kwa kukumbusha suala hili muhimu na adhimu kwa Taifa.

Tunatoa mwito kwa viongozi wengine wa serikali, dini, vyama vya siasa na vya kijamii na wananchi mmoja mmoja kuendelea kumuunga mkono Dk. Nchimbi kwa kukumbusha na kuonya kwa yeyote atakayeashiria kutaka kuuteteresha umoja wetu.

# HOSPITALI YA TEMEKE WAFIKIWA NA MISAADA KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE




NA MWANDISHI WETU

WAKATI dunia ikielekea kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, 2025, wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya ALAF wametoa vifaa mbalimbali muhimu kwa wodi ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Temeke, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya zoezi la utoaji wa vifaa hospitalini hapo, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Kampuni ya ALAF, Bi Hawa Bayumi alisema mpango huo ni wa wafanyakazi wanawake wote ambao walichangia kutoka mifukoni mwao kwa ajili ya mpango huo na kupata muda wa kujumuika na baadhi ya wagonjwa katika wodi ya wazazi.

"Mpango huu, ambao ni sehemu ya maandalizi ya Siku ya Wanawake Duniani Machi 8, unaendana na juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan za kuweka mazingira safi na salama kwa akina mama na watoto hospitalini, kuimarisha afya na ustawi wao," alisisitiza.

Aidha, alisema kwamba mchango wao huo unaonyesha moja kwa moja kujitolea kwao kwa maadili ya msingi ya kutoa huduma na ubia wa kampuni.

Kulingana na Bi Hawa, ishara hii inalingana na dhamira ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake mwaka 2025, "Harakisha Kuchukua Hatua," inayoonyesha umuhimu wa hatua za haraka na zenye matokeo ya kusaidia afya, usalama na uwezeshaji wa wanawake.

Kwa upande wake, Meneja Rasilimali Watu wa Kampuni ya ALAF Jumbe Onjero aliwapongeza wafanyakazi wanawake kwa kuwajali wanawake wenzao wanaohitaji msaada ili kuhakikisha wanajifungua salama.

"Kwa kutoa vifaa hivi muhimu vya usafi, wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya ALAF wanalenga kuleta matokeo ya maana na yanayoonekana katika jamii, kusherehekea nguvu na ujasiri wa wanawake," alisema Meneja wa Rasilimali Watu.

Alisema kupitia juhudi hizi na nyinginezo, wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya ALAF wanashiriki kikamilifu katika kuchangia harakati za kimataifa za maendeleo ya wanawake.

Wakati huo huo, Ofisa Ustawi wa Jamii wa Hospitali ya Rufaa ya Temeke, Bi Grace Samson Wella, aliwashukuru wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya ALAF kwa ukarimu huo na kusema msaada huo utawasaidia sana wanawake wakati wa kujifungua, hasa wale wasio na uwezo kifedha wa kumudu vifaa hivyo.

"Tunatoa wito kwa wanawake wengine kuiga kile ambacho wafanyakazi wanawake wa Kampuni ya ALAF wamefanya na nina hakika tutaokoa maisha mengi huko nje," alisema.

ALAF Limited ni kampuni inayoongoza nchini Tanzania kutengeneza vifaa vya chuma vya kuezekea majengo.

Baada ya kuanzishwa mwaka 1960, imekukuwa muda wote mdau muhimu katika maendeleo ya sekta ya ujenzi nchini.

Kampuni ya ALAF si tu huzalisha vifaa vya kuezekea vya chuma, lakini pia vifaa vingine mbalimbali vya ujenzi na mabomba kwa matumizi mbalimbali.

*Matukio mbalimbali ya picha katika ufunguzi rasmi wa Kongamano na Maonesho ya Petroli Afrika Mashariki (EAPCE'25) linalofanyika kwa siku tatu Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam. Ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, jana.*









*Matukio mbalimbali ya picha katika ufunguzi rasmi wa Kongamano na Maonesho ya Petroli Afrika Mashariki (EAPCE'25) linalofanyika kwa siku tatu Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam. Ambapo mgeni rasmi alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, jana.*

# HAKI ZA BINADAMU ZINAVYOKUWA TETE ULIMWENGUNI



NA MWANDISHI WETU

KATIKA Mkutano wa 58 wa Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu unaoendelea mjini Geneva Uswisi, Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Binadamu.

Volker Türk, amezungumzia hali ya kuzorota na kutoeleweka inayohusu haki za binadamu duniani kote akielezea wasiwasi mkubwa kuhusu kudhoofika kwa makubaliano ya kimataifa kuhusu haki hizo, na kuonya kwamba ushawishi wa viongozi wa kiimla, matajiri wakubwa, na viongozi wa kimabavu unatishia kuvuruga maendeleo ya miongo kadhaa.

Katika taarifa yake Türk amesisitiza umuhimu wa kuhifadhi haki za binadamu na utawala wa sheria ili kuzuia kurudiwa kwa ukatili wa zamani.

Moja ya masuala ya dharura yaliyotiliwa mkazo na Türk ni mgogoro wa kibinadamu unaoendelea huko Gaza. Amelaani uharibifu uliosababishwa na hatua za kijeshi za Israeli dhidi ya mashambulizi ya Oktoba 7, 2023 yaliyofanywa na Hamas na makundi mengine ya wapiganaji wa Kipalestina.

> *Ameihimiza jumuiya ya kimataifa kufanya kazi kuelekea amani endelevu inayoheshimu haki na matarajio ya watu wa Ukraine.*

Ibrahim al-Ghandour mkazi wa Gaza alisema kuwa, haoni kama kuna nia ya watu kuzingatia haki yao ya mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhani Gaza

Türk amesisitiza haja ya kudumisha usitishaji mapigano na kutoa wito wa mchakato wa amani unaozingatia haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na haki ya kujitawala na uwajibikaji. Ametaka kuachiliwa kwa mateka, kukomeshwa kwa vizuizi vya kiholela, na kuanza tena kwa msaada wa kibinadamu mara moja ndani ya Gaza.

Kuhujsu mgogoro unaoendelea nchini Ukraine amesema bado ni suala la kutia wasiwasi, huku raia wakiishi kwa hofu ya mara kwa mara kutokana na mashambulizi yasiyokoma.

Amekemea vikali vikwazo vya Shirikisho la Urusi juu ya haki za msingi katika maeneo yanayokaliwa kwa mabavu na kuelezea masikitiko yake kuhusu ripoti za mauaji ya kiholela na mateso ya kimfumo ya wafungwa wa vita wa Ukraine.

Ameihimiza jumuiya ya kimataifa kufanya kazi kuelekea amani endelevu inayoheshimu haki na matarajio ya watu wa Ukraine.

Türk pia ameelekeza mawazo kwenye maeneo mengine yenye migogoro, ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo DRC, Myanmar, Haiti, na Sudan. Ameelezea jinsi watawala wa kiimla, wanasiasa wahubiri wa chuki, na walanguzi wanavyotumia machafuko kwa faida zao binafsi.

Ametoa wito kwa watu binafsi kutambua jukumu lao la pamoja kwa kufanya maamuzi ya kimaadili ya ununuzi, kushiriki kisiasa, na kuunga mkono uwajibikaji kwa ukiukwaji wa haki za binadamu.

Hata hivyo alisema kuwa, demokrasia zilizoimarika haziko salama dhidi ya kudorora kwa haki za binadamu. Turk ameelezea wasiwasi mkubwa kuhusu mwelekeo nchini Marekani, ambako maendeleo kuhusu usawa wa kijinsia na sera za kupinga ubaguzi yanarudi nyuma.

Pia amekosoa Shirikisho la Urusi kwa ukandamizaji wake wa jamii za kiraia na vyombo vya habari huru, ambapo wapinzani wanakabiliwa na unyanyasaji, kukamatwa, au kufurushwa.

Kudhoofika kwa haki za binadamu katika mataifa yenye nguvu, Türk ameonya kwamba kunaweka mfano hatari kwa ulimwengu mzima, akisisitiza hitaji la dharura la mshikamano wa kimataifa na uwajibikaji kuhusu haki za binadamu.

# IDJWI: ENEO LILOPO KATIKATI YA VITA GOMA LIKIWA SHWARI



NA MWANDISHI MAALUM

KISIWA cha Idjwi nchini Kongo ni eneo lililosahaulika ambalo limeishi kwa miongo kadhaa ya vita bila kuathirika.

Kisiwa cha pili kwa ukubwa kilichoko ziwani barani Afrika, Idjwi, kipo katika sehemu ya kusini ya Ziwa Kivu, kikizungukwa na nchi mbili ambazo zimekuwa katika vita kwa karibu miongo mitatu, DRC na Rwanda.

"Hatuna wanajeshi hapa, kutoka upande wowote. Hatujawahi kusikia milio ya bunduki au mabomu, lakini tunahisi athari za vita," anasema Yves Minani, mjasiriamali na mkurugenzi wa kituo cha redio cha ndani.

Maisha kwenye Idjwi yanaelezwa kuwa ya amani, na mazuri. Ni tofauti kabisa na sehemu za bara ambako waasi wa M23 wanaoungwa mkono na Rwanda wameteka miji miwili mikuu ya mkoa, Goma na Bukavu.

"Tangu mwanzo hapa, hakujawahi kuwa na vita," anasema Mustafa Mamboleo, msimamizi wa eneo la Idjwi na afisa wa Kivu Kusini.

"Lakini hofu inaenea miongoni mwa wakazi kwani kufungwa kwa benki na mizozo sehemu za bara kunamaanisha bidhaa muhimu pia hazitufikii."

Kisiwa hicho ni makazi ya watu wapatao 300,000 Wengi wao, ni jamii ya Wahavu ambao wameishi hapa kwa miongo kadhaa.

Hakuna umeme au maji ya bomba na huduma za afya ni ngumu kupatikana. Hata hivyo, watu wanaokimbia vita katika Mashariki ya DRC wanaona ni mahali salama.

Kuna huduma chache kwa wakazi 300,000 wa Idjwi

Kufuatia mapigano makali katika mji mkuu wa Kivu Kaskazini, Goma, na maendeleo yasiyo ya kawaida ya waasi wa M23 katika mkoa wa Kivu Kusini, makumi ya maelfu ya Wakongo waliokimbia makazi yao wamekimbilia Idjwi.

Sasa wanalala katika kambi za wakimbizi zisizo rasmi kaskazini mwa kisiwa hicho, wakitegemea tu ukarimu wa wenyeji kwa msaada.

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, kuna angalau watu 42,000 wanaoishi katika kambi za muda, lakini hakuna rekodi rasmi kwa wale waliokolewa na familia za wenyeji. Wenyeji wanakadiria kuwa kunaweza kuwa na wakimbizi wengi kama 60,000 wanaoishi Idjwi.

"Hukuna kaya hapa ambayo haijampokea mwanafamilia, rafiki, au jamaa wa mbali aliyekimbia vita," anasema Yves Minani.

Vituo vya wakimbizi vimeanzishwa katika makanisa, shule na majengo yaliyotelekezwa. Mbali na jenereta chache, hakuna umeme au maji ya bomba.

Kuna hospitali kuu moja tu, na kuna magari machache tu, mara nyingi haiwezekani kwa wale walio katika maeneo ya mbali kupata matibabu.

"Wakati mwingine tunalazimika kutembea kilomita 10 na mgonjwa kwenye machela," anasema Yves. "Wakati mwingine wanakufa njiani kwa sababu hatuwezi kufika kwa haraka vya kutosha."

Licha ya kuwa na rasilimali chache, hii sio mara ya kwanza kwa wakaazi wa kisiwa hicho kufungua milango yao kwa wale watu wenye shida. Katika miaka ya 1990, wimbi la wakimbizi wa Rwanda lilifika Idjwi kukimbia maafa ya mauaji ya kimbari nyumbani kwao.

"Hiyo ndiyo Idjwi, hatuna makubwa watu, lakini tunakaribisha," anasema Yves.

Wakati wa Vita vya Kwanza na vya Pili vya Kongo vilivyoharibu eneo hilo katika miaka ya 1990, pia vinajulikana kama Vita vya Dunia vya Afrika, Idjwi ilikuwa sehemu salama.

Wenyeji wanasema mfululizo wa mazungumzo na vikundi vya waasi na vikosi vya jeshi viliwazuia kuingia kwenye mzozo.

"Tulisikia tu kuhusu vita kwenye redio au mara kwa mara wakati sauti ilivuka ziwa," anasema Yves.

Wakazi wengi wa Idjwi wanategemea kilimo cha kahawa, mihogo na nanasi

Wenyeji wanasema wanahisi wametelekezwa kabisa na serikali kuu iliyo umbali wa kilomita 1,545.

Mpango wa kitaifa wa kuleta umeme Idjwi ulianza mwaka 2006, lakini vifaa vilivyosafirishwa hadi kisiwani havikuwahi kufungwa.

"Vimeachwa tu vioze," anasema Yves. "Utafiti wote muhimu ulifanywa, pamoja na tafiti za topografia."

Lakini, licha ya kuonekana kama wamekwama katika wakati, Idjwi imevutia wengi wa wajasiriamali wanaojaribu kuboresha maisha ya wakaazi wa kisiwani.

Mnamo 2017, mradi kabambe ulileta mtandao wa kwanza wa WiFi (internet) kisiwani, unaoendeshwa na umeme wa jua (sola). Uliongozwa na Patrick Byamungu kutoka shirika linaloitwa 'La Différence.

Mtandao ulijengwa kwa kutumia miundombinu na vifaa vya ndani na unafadhiliwa kwa sehemu na biashara za ndani zinazolipa kutumia mtandao kabla ya saa 12 jioni, baada ya hapo ni bure kwa wakaazi wengine kutumia.

"Jioni, unaona kweli vijana, walimu, madaktari, wote wakikusanyika karibu na sehemu ya muunganisho ili kupata intaneti, mitandao ya kijamii, au kupiga simu tu kwa familia zilizo mbali," anasema Patrick.

Hii pia imesaidia kuunganisha wakaazi wa Idjwi wenyewe kwa wenyewe na pia kwa ulimwengu wa nje. Kama matokeo, ushirika unaokuza kahawa umeweza kusafirisha mazao yake kwa mashirika makubwa ya kimataifa kama Starbucks.

La Différence pia imefanya kazi na mamlaka za kisiwa kwenye miradi ya kijamii kama usajili wa kuzaliwa kidijitali na mpango wa uzazi wa mpango unaohusisha vikundi vya wanawake na watoa huduma za afya wa ndani. Hiyo ni njia nyingine ya kuleta msaada.

Wananchi wa Idjwi wanaishi kwa kutegemea ardhi. Kilimo cha ushirika cha mananasi, kahawa, na mihogo kimetengeneza ajira na fursa, na kuwapa wakazi wanaoongezeka njia ya kuishi.

Hata hivyo, takriban 80% ya wakaazi wa kisiwa hicho wanaishi chini ya dola moja kwa siku, maisha bado ni magumu. Biashara na sehemu za bara ni chanzo muhimu cha mapato.

"Biashara kati ya kisiwa hiki na Rwanda ni ya muda mrefu sana," anasema Padri Adrien Cishugi, ambaye ana nyumba kisiwani na anatumia muda mwingi huko kusaidia jamii ya Wapigmi.

Anasema kwamba katika baadhi ya sehemu za kisiwa, hasa kusini, watu hutumia zaidi faranga ya Rwanda kuliko faranga ya Kongo kwa sababu biashara yote inafanywa na Rwanda.

Kuna safari za mara kwa mara zinazounganisha miji ya Goma na Bukavu na Idjwi, na safari inachukua saa mbili hadi tatu.

Mwishoni mwa Januari, mapigano kati ya M23 na jeshi la Kongo yalisimamisha safari hizi, na kukinyonga kisiwa.

"Bila boti, maisha hayapo hapa," anasema PadreiAdrien Cishugi.

Bandari ya Goma ilipofungwa Januari baada ya wanajeshi wa M23 kuuteka mji, safari zote za boti zilisimamishwa. Lakini "walifanya msamaha maalumu kwa kisiwa kwa sababu kilikuwa matatizoni," anasema Padri Adrien.

Urithi wa kiasili

Biashara pia ndiyo inayowapa jamii ya Wapigmi wa Idjwi njia ya kujikimu.

Waliishi kama wawindaji katika misitu ya kisiwa hicho kwa maelfu ya miaka lakini walifukuzwa kutoka ardhi yao ya asili ili kutoa nafasi kwa ongezeko la idadi ya watu wa kabila la Bantu. Wengi walipoteza riziki zao kutokana na hilo, wakisukumwa kuishi pembezoni mwa jamii.

Kundi la kiasili la Wapigmi wa Idjwi, Bambuti, ni miongoni mwa watu wa kiasili wa zamani zaidi wa Afrika ya kati, lakini mara nyingi wametengwa na kutengwa na elimu ya kawaida.

Maelezo ya picha,Padri Adrien Cishugi amekuwa akifanya kazi na jamii ya kisiwa hichi kuboresha maisha yao

Tangu miaka ya 1990, Padri Adrien Cishugi amefanya kazi kwa pamoja na jamii hiyo kutengeneza fursa na kuboresha viwango vya chini vya kusoma na kuandika.

Amesaidia kuanzisha shule kwa watoto wa Wapigmi nje ya mfumo wa elimu wa kawaida.

Watoto huhudhuria masomo siku za Jumapili badala ya Alhamisi, ambayo kiasili ni siku ya soko kwa jamii yao. Ili kuwahimiza wabaki shuleni, wanapewa mlo kila siku na nguo safi.

Watoto hujifunza masomo ambayo Padri Cishugi anasema, "yanaendana na falsafa yao", kama vile dawa za kiasili, ufinyanzi, na usukaji wa vikapu.

"Katika programu za elimu za kitaifa, kuna masomo ya TEHAMA, lakini unawezaje kumfundisha TEHAMA mtu ambaye hajawahi hata kuona simu?" anasema.

# SERIKALI ILIVYOFAFANUA JUHUDI ZAKE KUPAMBANA NA UPUNGUFU WA AJIRA NCHINI

NA MWANDISHI WETU

MSEMAJI Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa amesema Serikali itaendelea kutoa nafasi ya ajira kwa wahitimu kila zinapopatikana, kwani siyo walimu pekee wanaokabiliwa na changamoto hiyo, bali hata tasnia nyingine kama waandishi wa habari.

Msigwa amesema hayo leo Machi Mosi, 2025 alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Tanga, mkutano wa tatu wa nchi zinazozalisha kahawa na uwasilishaji taarifa juu ya miaka minne ya Samia madarakani.

Msigwa ametoa kauli hiyo siku chache tangu walipoibuka viongozi wa umoja wa walimu wasiokuwa na ajira Tanzania kuanzia mwaka 2015 hadi 2023 (Neto), wakiwamo mwenyekiti, Joseph Kaheza na katibu, Daniel Edgar katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, wakitaka mambo kadha ikiwa ni pamoja na kusitishwa usaili wa kada ya ualimu, utaratibu ambao Serikali imeanzisha hivi karibuni.

Akizungumza na wanahabari, Msigwa mbali na kueleza Serikali imekuwa ikitoa ajira za walimu kwa awamu kila mwaka pia amesema anashangazwa kusikia viongozi wa Neto walikamatwa na Jeshi la Polisi baada ya kuzungumza na wanahabari. "Lakini walimu ambao hawajapata ajira si kwamba Serikali haijui inatambua na itaendelea kuajiri kwa namna ambavyo nafasi inaruhusu, kwa sababu tukisema tukimbilie kuajiri watu wote itabidi tuchukue hela za dawa, za maji, barabara ukalipe mishahara ya walimu," amesema.

Amesema Tanzania hakuna tasnia ambayo watu wake wengi hawajapata ajira akitoa mfano wa waandishi wa habari wanaozalishwa kila mwaka ni zaidi ya 500 jambo ambalo pia lipo katika tasnia nyingine. "Wapo maofisa maendeleo ya jamii hawajapata ajira, wako wahandisi, wachumi, wanasheria wengi, hivyo Serikali itaendelea kuajiri kila nafasi inapopatikana.

Haitawezekana kila anayehitimu chuo aajiriwe, itakuwa ni Serikali ya kulipa mshahara. "Maelezo yangu haya hayana maana ya kubeza madai ya walimu, yanafanyiwa kazi itakapokamilika mtajulishwa," amesema.

Uhaba wa walimu Mwaka 2023, madarasa ya awali na msingi pekee yalikuwa yanahitaji walimu zaidi ya 116,885 ili kuweka sawa uwiano wa walimu ikilinganishwa na wanafunzi waliokuwa wamedahiliwa.

Kwa mujibu wa Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa 2023 kilichotolewa na Wizara ya Fedha, Juni 13, 2024 madarasa ya awali yalihitaji walimu 52,884 na shule za msingi zilihitaji walimu 64,001 ili kuwa na uwiano uliopangwa na Serikali.

Takwimu zinaonyesha, madarasa ya awali mwaka 2023 yalikuwa na walimu 9,608 pekee ikilinganishwa na uhitaji wa walimu 62,491 katika mwaka 2023 ambao walipaswa kufundisha wanafunzi 1,562,286.

Kwa mujibu wa uwiano wa Serikali, walimu waliokuwapo walifundisha wanafunzi 163 ndani ya darasa moja ikiwa ni mara sita zaidi ya kiwango kilichowekwa na Serikali cha kufundisha wanafunzi 25.

Hata hivyo, idadi ya walimu wa madarasa ya awali waliokuwapo mwaka 2023 ni pungufu kwa asilimia 4.8 kutoka wanafunzi 10,093 waliokuwapo mwaka 2022. Idadi hiyo ya walimu ilishuka katikati ya ongezeko la wanafunzi kwa asilimia 8.8.

Hiyo ni baada ya wanafunzi katika shule za awali za Serikali waliodahiliwa kufikia 1,562,286 kutoka wanafunzi 1,435,735 mwaka 2022. Kitabu hicho cha hali ya uchumi kinaeleza idadi ya wanafunzi katika shule za Serikali




Inaendelea Uk. 13

# SERIKALI ILIVYOFAFANUA JUHUDI ZAKE KUPAMBANA NA UPUNGUFU WA AJIRA NCHINI

Inatoka Uk. 12

ilikuwa milioni 10.82 mwaka 2023 ambayo ilikuwa ikihitaji zaidi ya walimu 240,541 ili kuweka uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45.

Badala yake shule hizo zilikuwa na walimu 176,540 ambayo ni pungufu ya walimu 64,001 kufikia uwiano halisi. Idadi ya walimu waliokuwapo mwaka 2023 ilikuwa ni ongezeko la asilimia 1.8 ikilinganishwa na walimu waliokuwapo mwaka 2022. Wahitimu waliopo Kuhusu wingi wa wahitimu,

Ripoti ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania 2023 (TCU) iliyotolewa Mei, 2024 inaonyesha kozi hiyo imekuwa ikiongoza kwa kutoa wahitimu wengi kuliko nyingine. Ripoti za miaka tofauti za TCU zinaonyesha mwaka 2023, walimu waliohitimu walikuwa 15,103,




mwaka 2022 walikuwa 15,335, huku mwaka 2021 wakiwa 14,050.

Idadi ya wahitimu inaakisiwa na wingi wa wanaodahiliwa na mwaka 2023/2024 kati ya wanafunzi 106,570 waliodahiliwa kuanza mwaka wa kwanza katika kozi 17 zilizoainishwa, waliochagua ualimu walikuwa 27,731.

Ripoti ya mwisho ya Mpango wa hiari wa nchi za Afrika kujitathmini (APRM) iliyotolewa mwaka 2013 ililitaja suala la ukosefu wa ajira miongoni mwa changamoto zinazotakiwa kutafutiwa ufumbuzi, lakini hadi sasa utekelezaji wa pendekezo hilo haujafanyika kwa ufanisi, hali inayosababisha kuongezeka kwa kundi la vijana wasio na ajira.

Julai 11, 2024 wakati wa mkutano wa awali kabla ya kufanyika kwa tathmini nyingine ya APRM, Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa kwa Wananchi (TCIB), Deus Kibamba alilieleza kuwa Tanzania ina cha kujifunza kwa kilichotokea katika nchi nyingine za Afrika, ikiwa ni matokeo ya vijana kukosa ajira.

Alisema nchi inapokuwa na vijana wengi wasio na ajira ni rahisi kushawishika kufanya mambo yasiyofaa, akitoa mfano wa maandamano yaliyofanywa na vijana wa Gen Z nchini Kenya na yanayofanana na hayo katika nchi nyingine za Afrika.

"Ripoti ya APRM 2013 ilieleza suala la ajira hasa kwa vijana ni bomu ambalo lisipotafutiwa ufumbuzi linaweza kutuharibia utulivu na amani ambayo tumekuwa nayo kwa miaka mingi. Sasa tunapoelekea kwenye maandalizi ya kufanya tathmini ya pili ni muhimu suala hili likapewa kipaumbele," alisema.





# SIMBA YAMTOLEA MACHO MWAMUZI

>> Inatoka uk. 16

kutoridhishwa, huku wenzao wa Yanga wakilifagilia.

Hata hivyo hakuna sababu inayotolewa na mashabiki wa Simba dhidi yake, badala yake Wekundu hao wa Msimbazi wanadai kutokuwa na bahati naye, licha ya kusifu uwezo wake.

Ikumbukwe Arajiga ndiye aliyepuliza kipyenga wakati Yanga ilipovuna kalamu ya ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Simba na hata ushindi wa mabao 2-1.

Yote kwa yote mchongo ndiyo uko hivyo, ambapo kwa sasa mashabiki wanasubiri siku hiyo ifike ili wakutane katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, huku wachezaji pamoja na viongozi wa benchi la ufundi kwa timu zote wakiviandaa vikosi vyao ili viwe imara tayari kupata ushindi katika mchezo huo.

# KASEJA APEWA KIBARUA KIZITO KAGERA SUGA

NA MWANDISHI WETU

KWA mara ya kwanza kipa maarufu nchini Juma Kaseja atasimama kama Kocha Mkuu akijaribu kukinusuru kikosi cha timu kongwe katika Ligi Kuu Kagera Suga,r isishuke daraja msimu huu.

Kaseja alikabidhiwa mikoba hiyo juzi na uongozi wa klabu hiyo yenye makao yake makuu mjini Bukoba, huku msimamo ukisoma kuwa ipo nafasi ya 15 katika msimamo wa ligi ikiwa ni ya pili kutoka mwisho.

Mpaka sasa Kagera imeshacheza mechi 22 ikishinda 3 na kutoka sare 7, kibindoni ikiwa na ponti zake 16 pekee.

Nafasi hiyo si salama sana kwa Wana 'Nkurukumbi' hao kwani Ken Gold iunayoburuza mkia ina jumla ya pointi 15 pungufu ya moja tu kuwa sawa na Kagera Sugar, huku timu iliyo juu ambayo nayo ipo katika zile tatu zilizopo katika mstari mwekundu ni Tanzania Prisons ambayo imecheza mechi 22 na kujikusanyia Pointi 18, nyongeza ya pointi mbili kutoka kwa Kagera.

Kwa vyovyote Juma Kaseja aliyewahi kuwa kipa mahiri wa vikosi vya Simba na Yanga pamoja na timu ya taifa hatokipokea cheo hicho kwa furaha kwani itambidi kupambana ili ainasue timu hiyo kutoka mkiani, ili aweze kuwa na uhakika wa kurudi tena kucheza Ligi Kuu ya NBC msimu ujao.





# P-SQUARE
## 'Mapacha' ndani ya mgogoro!-5

LOGOS, NIGERIA

Ni lazima ieleweke kwamba mashabiki hawakupenda P-Square kwa sababu ya nani aliimba au kucheza zaidi. Kilichotufanya tufanikiwe ni ubora wetu hali yetu iliotokana na juhudi zetu za pamoja – sisi wawili! P-Square ilikuwa ya nguvu, na mashabiki waliipenda P-Square kwa sababu ya upekee wetu na umoja, "aliongeza.

Pia alimkosoa Paul kwa kujilinganisha na Jude, akisema kuwa mienendo ya familia ilikuwa na jukumu kubwa katika matatizo ya bendi. "Ulimvunjia heshima mke wangu, familia yangu, kipaji changu, mawazo yangu na hata kuchukua upande wa Jude wakati alipokuwa anajaribu kunikandamiza."

Katika kukamilisha ujumbe wake, Peter alielezea kusikitishwa kwake na hali ya sasa na athari ambayo P- Square imekuwa nayo kwa mashabiki wao. "Sasa nahisi kama umechukua mambo hata zaidi kwa kujaribu kuwageuza mashabiki dhidi yangu kwa kuwafanya wafikiri nina wivu kwako. Umefanya kila kitu unachoweza kuwafanya mashabiki wanichukie, lakini unajua nini? Hawatanichukia kamwe; badala yake, watatuchukia sisi sote kwa sababu tuliwavunja moyo na kuwaangusha."

# DRAKE AFICHUA SIRI YA MAFANIKO YAKE



LOS ANGELES, MAREKANI

SUPASTAA wa muziki wa Hip hop, Drake, amesema siri ya mafanikio yake ni kujifunza kutoka kwa waliofanikiwa.

Drake mwenye umri wa miaka 38, amesema tangu alipokuwa mdogo, alipenda kufuatilia maisha ya mastaa na kuvutiwa na hatua zao kwenye maisha.

Mshikaji huyo mzaliwa wa Toronto, alianza rasmi safari yake ya muziki mwaka 2006 kupitia 'mixtape' yake ya 'Room for Improvement.'

# Tamasha la muziki 'Kadanse ya Mama' yakumbusha enzi za Gurumo na Bitchuka

NA MWANDISHI WETU

TAMASHA la Muziki wa dansi lililoitwa Kadanse ya Mama lilifanyika juzi Jumamosi katika Viwanja vya Ledrs Kinondoni Jijini Dar es Salaam na kushudiwa na umati wa mashabiki huku bendi zaidi ya kumi zikitumbuiza.

Miungoni mwao ni bendi kongwe Msondo Ngoma Music Band iliyoazishwa tangu mwaka 1964 pamona na Mlimani Park iliyozaliwa mwaka 1978, bendi hizi zilipitiwa na wanamuzki mbalimbali wakiwemo maarufu Muhidin Maalim Gurumo ambaye ameshatangulia mbele ya haki na Hassan Rehani Bitchuka ambaye kwa sasa amepumzika masuala ya muziki.

Wanamuziki hao wanakumbukwa kutokana na kila bendi kati ya hizo mbili kuwa na wanamuziki wanaonakiri sauti zao na hivyo kusikika kama wakongwe hao walikupo jukwaani.

Ttukiacha historia ndefu ya jinsi waimbaji wawili nguli Muhidin Gurumo na Hassan Bitchuka walivyokutana kwa mara ya kwanza mwaka 1973 katika bendi ya NUTA Jazz, baadaye wakakutana tena katika miaka na bendi tofauti, lakini mkutano wao wa mwaka 1991 ulikuwa na kishindo kikubwa.

Mwaka huu miamba hii ilikutana tena katika bendi ya Juwata Jazz, hii ni baada ya misele ya kuingia na kutoka mfano kwenda Mlimani park na kisha Orchestra Safari Sound, hapa walikutana tena.

Tena basi katika mkutano huo mabingwwa hawa wa uimbaji hawakuwa hao wawili tu, bali waliwakuta wenzao waliokwisha jijingea mahaba makubwa kwa mashabiki kutokana na uwezo wao wa kuimba na pia tungo zao bora.

Katika safu ya uimbaji pia alikuwepo TX Moshi William, Joseph Maina, Juma Akida, Isaya Swahiba, Athuman Momba, Joseph Lusungu na Hamisi Kitambi.

Kipindi hicho Juwata jazz 'Wanamsondo ngoma' ilikuwa ikihudumiwa na wanamuziki takriban 28 wakiwemo na mafundi mitambo.

Tarehe 5.9.1991 bendi hii ilikuwa imekamilisha mazoezi ya nyimbo 9, na kuingia Studio za RTD kwa ajili ya kuzirekodi.





UK. 15

tanzaniabora @tanzaniabora @tanzaniabora

Tanzania BORA MICHEZO

ALHAMISI Machi 06, 2025

Tovuti: www.tanzaniabora.co.tz

# Simba yamtolea macho mwamuzi



NA MWANDISHI WETU

HAKUNA ubishi kwamba Simba na Yanga ni rasmi sasa zitaonyeshana ubabe katika mchezo wa Ligi Kuu ya NBC, utakaopigwa Jumamosi Machi 8, huku mwamuzi wa mchezo huo akitajwa kuwa ni Ahmed Arajiga.

Refa huyo kutoka Manyara atakuwa akiandika rekodi ya kuchezesha mechi ya watani hao mfululizo baada ya kufanya hivyo katika mechi tatu zilizopita. Muda mfupi baada ya Bodi ya Ligi kumtaja Arajige kama mwamuzi wa kati katika mechi hiyo, mashabiki wa timu hizo wamelipokea jina hilo kwa hisia tofauti, huku wale wa Simba wakionyeshwa

Inaendelea Uk.14

# KASEJA APEWA KIBARUA KIZITO KAGERA SUGAR



NA MWANDISHI WETU

KWA mara ya kwanza ya kipa maarufu nchini Juma Kaseja atasimama kama Kocha Mkuu akijaribu kukinusuru kikosi cha timu kongwe katika Ligi Kuu Kagera Suga,r isishuke daraja msimu huu.

Kaseja alikabidhiwa mikoba hiyo juzi na uongozi wa klabu hiyo yenye makao yake makuu mjini Bukoba,

Inaendelea Uk.14

# TIKETI MECHI YA SIMBA, YANGA ZAADIMIKA MTAANI

NA MWANDISHI WETU


WAKATI zikisalia siku mbili kabla ya kufanyika mpambano wa kihistoria kati ya timu pendwa za Tanzania, Simba na Yanga kasi ununuzi wa tiketi kwa ajili ya mchezo huo inakwenda mbio za nyikani.

Hadi kufikia jana asubuhi kupitia ukurasa wa Yanga ilitambusha kununuliwa kwa tiketi zote za VIP na hivyo mashabiki wakaanza kuhamasishana ili kuzifagia zilizobaki.

Tiketi zilizokuwa zikiendelea kununuliwa kwa kasi tangu jana ni pamoja na VIP B, C, Orange na Mzunguko, ambapo gazeti hili halijapata taarifa mpya kama ziliendelea kuwepo katika vituo au zilishamalizika

Mchezo huo unaovuta hisia kwa mashabiki wa soka nchini, unatarajiwa kupigwa katika dimba la

Inaendelea Uk.14



GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM